SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 2 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I2.4026

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA METHALI KATIKA MASHAIRI YA SAADAN KANDORO

*Hamad Jabir Bashir & Mohamed Omary Maguo

Department of Linguistics and Literary Studies, Faculty of Arts and Social Sciences, The Open University, Dar es Salaam, Tanzania.

**Keywords:**
Maadili
Kujenga
Elimu
Mbinu ya usomaji
Jina la shairi

**A B S T R A C T**

Makala haya yanahusu kuchunguza matumizi ya methali katika mashairi ya Saadan Kandoro kupitia diwani ya Mashairi ya Saadani. Methali ni kipera katika utanzu wa semi ambacho ni kipera kikongwe kinachotumika katika jamii kujenga maadili na kutoa elimu kwa watu wote. Methali zinapatikana katika kila jamii duniani popote pale anapoishi mwanadamu. Makala haya yamekusanya data kutoka katika diwani teule ya Mashairi ya Saadani kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo na nadharia ya Simiotiki. Makala yamebaini kwamba, methali katika mashairi ya Saadani Kandoro yanatumika kama jina la shairi, ndani katika beti za mashairi, kama kibwagizo na kama mwangwi.

# دراسة استخدام الأمثال في قصائد سعدان كندورو

*حمد جبر بشير و محمد عمري ماجو

قسم اللغويات والدراسات الأدبية، كلية الآداب والعلوم الاجتماعية، الجامعة المفتوحة، دار السلام، تنزانيا.

**الكلمات المفتاحية:**
الأخلاق
البناء
التعليم
تقنية القراءة
اسم القصيدة

**الملخص**

تتناول هذه المقالة دراسة استخدام الأمثال في قصائد سعدان كاندورو من خلال مجلس الشعر السعداني. المثل هو مثل في لغة الكلام، وهو مثل قديم يستخدم في المجتمع لبناء الأخلاق وتوفير التعليم لجميع الناس. توجد الأمثال في كل مجتمع في العالم، أينما يعيش البشر. وقد قامت هذه المقالة بجمع البيانات من مجموعة مختارة من قصائد السعداني باستخدام أسلوب القراءة المتأنية وتحليلها باستخدام الأساليب الوصفية ونظرية السيميائيات. وقد أشار المقال إلى أن الأمثال في قصائد سعداني كاندورو تُستخدم كعنوان للقصيدة، وفي أبيات القصائد، وكقافية، وكإشارة .

## 1.1 Utangulizi

Methali ni semi ambazo hutumika kutoa mafunzo kwa jamii tangu hapo kale mpaka hivi leo (Kunemah, 2008). Methali huhusishwa kwa kiasi kikubwa na watu wenye umri mkubwa kwa sababu ndiyo wanadaniwa kuwa na busara na hekima katika jamii kuliko vijana na watu wa marika (Mulokozi na Kitogo, 2007). Methali huwasilisha maneno na misemo yenye busara na mafunzo ndani yake kwa lugha fupi iliyo na muundo wa kishairi. Itakumbukwa kwamba, methali zilianza kutumiwa na wanajamii katika kipindi cha usimulizi wakati ambapo hakukuwapo maandishi. Kwa hivi muundo wa methali kuwa ni wa kishairi ilikuwa ni namna muhimu ya kuwezesha methali kukaririwa katika akili ya mwanajamii na kuitumia mara kwa mara.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa, muundo wa methali za Kiswahili kuwa ni wa kishairi ni njia muafaka ya kutoa msisitizo kwa msikilizaji au mwelezwaji wa methali juu ya jambo maalumu. Kwa mfano, "haba na haba hujaza kibaba", katika methali hii tunaona silabi "ba" ikirudiwa mara mbili katika kipande cha kwanza cha methali na mara mbili tena katika kipande cha pili. Hii yote inaonesha kwamba, suala la kuweka mali kidogokidogo ni muhimu kwani siku moja ikifika mali hiyo itakuwa nyingi. Vilevile, inasisitiza kwamba, mtu hawezi kupata mali nyingi kwa mara moja bali ni sharti awe na tabia ya kuweka kidogokidogo.

Maitaria (1991) anaeleza kwamba, kutokana na umuhimu wa elimu itolewayo kwa jamii kupitia methali, hata katika vitabu vitakatifu hususani Injili au Biblia yapo matumizi ya methali ambazo zimejaa mafunzo yenye busara na hekima ndani yake. Kutumika kwa methali katika vitabu vitukufu ni ishara kwamba, methali ni semi zilizo na umuhimu mkubwa katika kufunza maadili mema kwa wanajamii wote. Kutokana na umuhimu huu wa methali imekuwa ni kawaida kuona waandishi wa mashairi, riwaya, tamthilia na hadithi fupi kutumia methali katika utunzi wa kazi zao ili ziweze kuwasilisha dhamira kama inavyopasa katika jamii (Senkoro, 2006). Si jambo la kawaida kusoma kazi ya fasihi andishi ya mtunzi fulani mwanzo mpaka mwisho pasipo kukutana na methali au msemo hata mmoja katika kazi yake. Senkoro (ametajwa) anasema kuwa ni vigumu mno kutenganisha tanzu za fasihi kwa kuwa zinategemeana na kushikamana katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira. Hivyo, kuzitenganisha tanzu za fasihi hufanywa kwa nia ya kujifunza tu na kufanya uchambuzi lakini katika uhalisia tanzu hizi hazitenganishiki

*Corresponding author:
E-mail addresses: hamadjabr90@gmail.com, (M. O. Maguo) Omarymohamed36@out.ac.tz

*Article History : Received 15 May 2025 - Received in revised form 18 November 2025 - Accepted 20 November 2025*

hata kidogo. Ukisoma shairi utakutana na tanzu nyingine nyingi ndani ya shairi ambapo kupitia tanzu hizo ndipo shairi linaweza kufikisha ujumbe wake kwa hadhira iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa na mtunzi.

Maitaria (2010) anasema kuwa methali zinaweza kutumika kama kichocheo cha kuibulia na kuwasilishia maudhui katika mashairi ya Kiswahili. Vilevile anasema kwamba, methali zinaweza kutumika kama mbinu ya kuibulia taharuki katika mashairi ya Kiswahili. Maelezo haya yanakubalika na kuaminika kitaaluma kwa kuwa hizi anazozitaja ni sehemu ya dhima za methali katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa hadhira ya mashairi ya Kiswahili. Mulokozi na Kitogo (2007) wanasema kwamba zaidi ya kuibua dhamira na taharuki methali na misemo ina dhima ya kuwasilisha utamaduni, falsafa na mitazamo mbalimbali ya maisha katika jamii zinapotumika katika mashairi. Tofauti na dhima chache za matumizi ya methali katika ushairi zilizotajwa na Maitaria (2010; 2012) makala haya yamechunguza matumizi ya methali katika ushairi wa Saadani Kandoro kupitia diwani yake ya *Mashairi ya Saadani* aliyoiandika mwaka 1972 tukiwa na lengo la kutaka kuona matumizi ya methali yanasaidiaje katika kujenga dhamira za diwani husika.

**2.1 Mkabala wa Kinadharia**

Nadharia ya Simiotiki ndiyo iliyotumika katika makala haya kwenye kufanya uchambuzi wa matumizi ya methali katika diwani ya *Mashairi ya Saadani*.

**2.1.1 Nadharia ya Simiotiki**

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuihakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002).

Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Chandler (1992) anaeleza kwamba, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa alama hizo. Wasomaji na watazamaji wa kazi za fasihi hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama hizo. Mawazo haya yanakamilishwa na yale ya Chandler (1992) aliposema kuwa, tunafikiri kwa kutumia alama. Alama hizo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda au yambwa. Anaendelea kueleza kwamba, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kama kirejelee, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (a signified), yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja, na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao.

Bathes (1994) akaja na aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Kiishara na Kiurejelezi.

Saadan Kandoro kwa kiasi kikubwa anaandika kazi zake ushairi kwa kutumia lugha ya picha, sitiari, taswira na misimbo ya aina mbalimbali katika kujenga dhamira mbalimbali kwa wasomaji na hadhira yake kwa jumla. Matumizi ya nadharia ya Simiotiki katika makala haya yametuwezesha kupata maana ya misimbo inayojengwa na methali katika mashairi ya Saadan Kandoro.

**3.1 Methodolojia ya Makala**

Makala ama utafiti wa kitaaluma huandikwa baada ya kukusanywa data na kuchambuliwa kwa kufuata misingi ya kisayansi (Kothari, 2008). Katika makala haya, data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Usomaji makini ni mbinu ya kuchambua data kwa mtafiti kusoma kwa makini matini aliyoiteua ili kupata kwa kuzingatia muongozo maalumu kutoka katika lengo la utafiti wake (Creswell, 2009). Kupitia mbinu hii ya usomaji makini, waandishi wa makala haya walizingatia hatua tano za ukusanyaji wa data kwa kusoma kwa makini mashairi ya diwani ya Mashairi ya Saadan. Hatua zilizozingatiwa ni pamoja na kwanza, msomaji alisoma mashairi ya diwani teule zaidi ya mara moja bila kunukuu au kuchukuwa dondoo lolote lengo likiwa ni kupata uelewa wa jumla kuhusu matumizi ya methalli katika diwani teule. Hatua ya pili ilikuwa ni kusoma na kuchukuwa madondoo ambayo ndani yake mnaonesha matumizi ya methali katika mashairi, hatua ya tatu ikawa ni kutengeneza vichwa ili ndani yake kuwekwe madondoo yenye data, hatua ya nne ikawa ni kuunganisha data kwa kuweka zinazofanana pamoja na kutenganisha zinazotofautiana na hatua ya tano nay a mwisho ikawa ni kuziweka data kwenye mpango rahisi wa kuzichambua. Kazi ya kukusanya data ilipokamilika, zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo ambapo data zote zilipatiwa maelezo ya kiuchambuzi yenye kukidhi lengo la makala haya.

**4.1 Matumizi ya methali katika diwani ya Mashairi ya Saadani**

Methali katika *Mashairi ya Saadani* zinatumika kwa namna mbalimbali katika kujenga dhamira kwa wasomaji wa mashairi ya mtunzi mahiri Saadan Abdul Kandoro. Makala haya yamebaini kwamba, matumizi ya methali katika diwani husika yanajitokeza kama jina la shairi,

**4.1.1 Methali kama jina la shairi**

Jina la shairi hapa tunarejelea mada ya shairi husika na imekuwa imeandikwa juu ya shairi na kisha ndio beti za shairi husika kuanza kutiririka. Katika diwani ya Mashairi ya Saadani zipo methali kadhaa ambazo ndizo zimekuwa ni mada ya mashairi husika. Takribani mashairi 11 yamebainika kuwa na methali kama ndio mada ya shairi na miongoni mwa mashairi hayo ni "Binadamu Tenda wema," ukurasa wa 18, Ada ya Ahadi Deni," ukurasa wa 27, "Hki Huvunja Milima," ukurasa wa 67 Panya Akitaka Jina," ukurasa wa 71, "Baada ya Kisa Mkasa," ukurasa wa 74, "Naisubiri Subira," ukurasa wa 76, "Usiku Ukikomaa Karibu Kupambazuka," ukurasa 77, "Utu ni Koja na Taji," ukurasa wa 79, "Chungu la Kovu si Donda," ukurasa wa 102-103, "Baada ya Dhiki Faraja," ukurasa wa 129, na "Safari ni Hatua."

Mashairi haya yote kwa idadi 11 yametumia methali kama mada au kichwa cha shairi husika na kufanya dhamira kuanza kujitokeza tangu katika mada ya shairi. Msomaji anaanza kuelewa maana ya au dhamira ya shairi kabla hata hajasoma beti za shairi husika na hapa ndipo msimbo wa Kihemenitiki wa nadharia ya Simiotiki unapofanya kazi yake. Kupitia msimbo huu msomaji anaweza kuelewa dhamira mapema kabisa na kuamua aendelee kusoma shairi au inatosha. Tuone mfano mmoja kutoka katika shairi la "Baada ya Dhiki Faraja," ambalo lipo ukurasa wa 129 ambalo limeandikwa hivi:

**BAADA YA DHIKI FARAJA**

Baada ya dhiki faraji, Muyaka alifumbua,
Kwa pepo za meleleji, hakuna lisilo kuwa,
Tawakali kwa mpaji, na safari itakuwa,
Muyaka alifumbuwa, baada ya dhiki faraja.

Baada ya dhiki faraji, Muyaka alifumbua,
Uendapo ngezi maji, kwa safari ya mashuwa,
Hapo ukumbuke mbiji, ya kutweka na kutuwa,
Muyaka alifumbuwa, baada ya dhiki faraja.

Kimsingi, shairi hili lina jumla ya beti 10 na zote zinashadadiwa na methali "Baada ya dhiki faraja," tangu katika mada na pia hata ndani ya beti methali inajitokeza. Hapa tunasema mtunzi ametumia mtindo wa msisitizo kuhakikisha kuwa hoja au dhamira ambayo anataka hadhira yake iipate basi inaipata bila kipingamizi chochote tena kwa uwazi kabisa. Mashairi yote 11 yaliyoandikwa kwa mtindo huu wa kuwa na methali kama ndio mada ya shairi husika umezifanya dhamira zake kujitokeza kwa urahisi na kueleweka haraka kwa wasomaji. Sasa tutazame matumizi ya methali kwenye beti kama sehemu ya ujitokezaji wa methali katika mashairi ya Saadani Kandoro.

**4.1.2 Methali kwenye Beti**

Tunachokusudia kubainisha hapa ni namna methali zilivyojitokeza ndani ya beti za mashairi kama sehemu ya ujitokezaji wa methali katika mashairi ya Saadani Kandoro. Katika uchambuzi wetu wa dhamira tumebaini kuwa kuna mashairi 5 ambayo yametumia methali ndani ya beti za mashairi hayo. Mashairi hayo ni "Tosheka na Upatacho, Usililie Dunia," ukurasa wa 15, "Ada ya Ahadi Deni," ukurasa wa 27, "Mwendo," ukurasa wa 35, "Mzigo Nimelemewa," ukurasa wa 101 na "Haina Siri Dunia," ukurasa wa 105. Mashairi haya yana matumizi ya methali ndani ya beti za shairi husika. Tutolee mfano shairi la "Mzigo Nimeelemewa," ukurasa wa 101:

**MZIGO NIMEELEMEWA**

Palipoingia kovu, haparudi kuwa sawa,
Na patendwe uerevu, madawa kupakaliwa,
Mabaya ni machukivu, magumu kuvumiliwa,
Mzigo nimeleewa, ninajitia udovu.

Maovu ni nimeemevu, Amri nimeelewa,
Nafanya ukakamavu, lakini nguvu zapowa,
Bado sijawa mpevu, sasa nitapevuliwa,
Mzigo nimeelemewa, ninajitia undovu.

Matumizi ya methali katika shairi hili yanajitokeza katika ubeti wa kwanza msitari wa kwanza na methali yenyewe ni "Palipoingia kovu, haparudi kuwa sawa." Methali hii imejitokeza kwenye ubeti huo tu na haijitokezi mahali pengine popote katika shairi zima. Kuwepo kwa methali hiyo kumetusaisia kuelewa dhamira ya shairi husika kuwa ni vema kuwashirikisha watu wengine katika kusaidiana kufanya kazi kuliko mtu kuhangaika peke yake katika kufanya kazi. Pia, methali hii inaelezea suala la mapenzi ambapo mtu akishapata masaibu ya mapenzi kama vile kutokuelewana na mpenzi wake basi hupata madhara katika moyo wake na hivyo kuwa vigumu kupona majeraha ya moyo. Hapa tumetumia msimbo wa kiseme wa nadharia ya ambayo imetusaidia kuelewa maana ya kovu kifasihi kama ilivyotumika katika shairi husika. Sasa tutazame ujitokezaji wa methali katika kibwagizo.

### 4.1.3 Methali katika Kibwagizo

Kibwagizo ni mshororo wa mwisho katika kila ubeti ambao unafanana katika beti zote za shairi zima. Kwa kiasi kikubwa mashairi mengi ambayo tuliona kichwa cha mada kikiwa ni methali na pia methali hizo zinajitokeza katika kibwagizo cha mashairi hayo. Jumla ya mashairi 9 yana matumizi ya methali kama kibagizo. Mashairi hayo ni "Soko," ukurasa wa 61, "Haki huvunja Milima," ukurasa wa 67, "Panya akitaka Jina," ukurasa wa 71, "Baada ya Kisa Mkasa," ukurasa 74, "Usiku ukikomaa Karibu Kupambazuka," ukurasa wa 77, "Utu ni Koja na Taji," ukurasa wa 79, "Chungu la Kovu si Donda," ukurasa 102, "Baada ya Dhiki Faraja," ukurasa wa 129, na "Safari ni Hatua," ukurasa wa 134. Katika mashairi haya kuna ujitokezaji wa methali katika vibwagizo na hapa tuone mfano ufuatao:

**WALA MSIKASIRIKE SAFARI INA HATUWA**

Umechafua upepo, manahodha msitweke,
Mtulie papo hapo, mpaka upepo utoke,
Hamtajuwa mwendapo, bahari ifanya teke,
Wala msikasirike, safari ina hatua.
…
Kaditama yangu basi, napenda mnasihike,
Kali dharuba ya kusi, make mpumzike,
Safari za wasiwasi, bora hasa zivunjike,
Wala msikasirike, safari ina hatuwa.

Methali hii imetumia kibwagizo cha methali "Safari ina hatua," ambayo ni methali inayoelezea kuwa safari ni hatua ikiwa na maana kuwa kila jambo hufanywa kwa kuzingatia taratibu maalumu na si vinginevyo. Uvumilivu ni jambo muhimu sana na kupitia methali hii ambayo imerudiwa katika kibwagizo inatoa msisitizo wa dhamira hii. Hii inamfanya msomaji kukutana na methali katika kila ubeti na hapo inamwingia zaidi na kuielewa kwa undani zaidi. Sasa tutazame ujitokezaji wa methali kama kiitikio.

### 4.1.4 Methali kama Kiitikio

Kiitikio ni mshororo wa mwisho katika kila ubeti kuwa tofauti na ubeti mwingine ikiwa na maana kuwa kila ubeti unakuwa na mshororo wa mwisho wa pekee. Katika shairi la "Mambo Yanapokutana," ukurasa wa 144.

Aha! Afia na watu, hakika yakikutana,
Watu pindi awe mtu, chakula kupatikana,
Furaha nyumbani mwetu, na tabia kulingana,
Aha! Umoja ni nguvu! Vigumu kushindikana.
…
Kutulizana na jembe, wawili mkikutana,
Huitwi mwanamkembe, jembe lolote hufana,
Kijijini na tuimbe, mikono tukishikana,
Aha! Wali na embe, kinywani vikikutana.

Tukiangalia beti hizi mbili tunaona kuwa ubeti wa kwanza na wa pili kila mmoja una mshororo wa mwisho ambao ni tofauti na wa pili. Kiitikio cha ubeti wa kwanza ndio chenye methali "Umoja ni nguvu," ambayo inahamasisha umoja na mshikamano katika jamii. Ingawa ubeti wa pili una kiitikio tofauti na ubeti wa kwanza lakini bado pia nao unajenga dhamira ileile ya umoja na mshikamano. Baada ya kuona methali ikijitokeza kama kiitikio sasa tuone methali ikijitokeza kama mwangwi.

### 4.1.5 Methali kama Mwangwi

Mwangwi ni sauti ambayo husikika katika ukumbi wenye uwazi mkubwa ikiwa na maana ukumbi mkubwa ambao hauna kitu ndani. Ni ukumbi au chumba ambacho ni ombwe na hivyo mtu au watu wanapoongea sauti hujirudia na kusikika na huo ndio huitwa mwangwi. Methali kama mwangi hujitokeza pale ambapo unaposoma beti za shairi na kuona methali fualani inajitokeza ingawa methali yenyewe hainekani kutokea bayana katika maandishi. Tuone mfano wa shairi la "Siafu Wamekazana" katika ukurasa wa 138 na hapa kuna mfano ufuatao:

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna,
Tena amekasirika, hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.
…
Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajua fika, siafu wakiungana,
Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,
Siafu wameungana, nyoka amekasirika.

Beti hizi mbili ni kati ya 6 za shairi hili na zinawasilisha dhamira ya umoja na mshikamano hasa katika kipindi cha kupigania uhuru. Methali ya "Umoja ni nguvu," inajitokeza hapa ambapo tunaona mdudu siafu ameungana na kufanikiwa kumuangamiza nyoka. Nyoka anayetajwa hapa ni mkoloni na siafu ni wananchi wakawaida. Wananchi wa kawaida walipoungana pamoja walikuwa na nguvu na kufanikiwa kumuondoa mkoloni licha ya kuwa alikuwa ni mtawala mwenye nguvu, mabavu na silaha nzito ikilinganishwa na wananchi wa kawaida. Hii inathibitisha methali ya Kiswahili ya kwamba "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu," na inatoa msisitizo kuwa umoja na mshikamano ni silaha muhimu ya maendeleo katika jamii.

### 4.2 Hitimisho

Makala haya yamefanikiwa kubainisha namna matumizi ya methali yanavyojitokeza katika diwani ya Mashairi ya Saadani ambapo imbainika kwamba, methali zimejitokeza kama jina la shairi, kwenye beti za shairi, kama kibwagizo na kama mwangwi. Matumizi haya ya methali yamesaidia kujenga dhamira mbalimbali kwa wasomaji wa mashairi husika. Vile vile, kupitia matumizi ya methali msisitizo wa dhamira umeweza kupatikana kwani msomaji anapokutana na methali ambayo wakati mwingine ameshakutana nayo basi inakuwa ni rahisi kuipata vizuri dhamira iliyokusudiwa na mtunzi wa shairi husika.

### MAREJELEO


Bathes, R. (1994) *The semiotic challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Chandler, D. (2001) *Semiotics*: *The basics*. London: Routledge.

Creswell, J. W. (2009) *Research Design: Qualitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Kandoro, S. A. (1972) *Mashari ya Saadani*. Dar es Salaam: NPL.

Kothari, C.R., (2008) *Reserch methodogy: Methods and techiniques* New Delhi: New Age Internationl Publising Ltd.

Kunemah, A. S. K. (2008) Misemo na methali katika ushairi. Dar es Salaam: TATAKI.

Maitaria, J. N. (1991) "Methali za Kiswahili kama chombo cha mawasiliano: Mtazamo wa kiisimu jamii," Tasinifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Maitaria, J. N. (2010) "Methali kama fomula ya uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili: Mfano wa baadhi ya mashairi ya Abdilatif Abdalla," Katika *Kioo cha Lugha Juzuu la Nane*, Dar es Salaam: TUKI. Kur. 107-117.

Maitaria, J. N. (2012) "Uainishaji wa ushairi wa Kiswahili: Dhima ya methali," Tasinifu ya uzamivu ya Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mulokozi, M. M. na Kitogo, S. (2007) *Mithali na Mifano ya Kiswahili-Shaaban Robert*, Dar es Salaam, TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (2006) "Fasihi ya Kiswahili ya majaribio: Makutano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi",

katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Wamitila K. W. (2002) *Uhakiki wa fasihi*: *Misingi na vipengele yyake*, Nairobi: Poenix Publisher Ltd.

Wamitila K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi*: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi. Nairobi: Vide – Muwa.